

# SAFARI YETU

*Toleo la Kwanza 2021*

FADev

TAASISI YA KUENDELEZA UCHIMBAJI MDOGO

## Ujumbe kutoka kwa Mwenyekiti



Safari yetu imekuwa ndefu na yenye malengo makubwa. Ni karibu miaka miwili sasa tangu FADev isajiliwe rasmi mnamo mwezi Julai mwaka 2019 kama Taasisi Isiyo ya Kiserikali yenye lengo la kuendeleza uchimbaji mdogo wa madini. Lakini safari yenyewe ilianza tangu mwaka 2016 wakati taasisi ya HakiMadini yenye makao yake makuu Arusha, Tanzania kwa kushirikiana na tasisi ya kimataifa inayohusika na mambo ya mazingira na maendeleo (IIED) walipoanza kuangalia mwenendo wa sekta ya uchimbaji mdogo wa madini nchini Tanzania. Huo ndio mwanzo wa historia ya FADev kama ilivoelezwa kwa undani katika ripoti hii. Tangu hapo, tumepitia hatua mbalimbali mpaka kusajiliwa kama Taasisi isiyo ya Kiserikali chini ya Sheria ya *"Non-Governmental Act, 2002)*

Kwa niaba ya Baraza la Uongozi la FADev, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wale wote waliowezesha FADev kuwepo na kuanza kufanya kazi. Kwanza kabisa, naomba kutoa shukurani za dhati kwa Serikali yetu ya Tanzania kwa kuweka mazingira wezeshi kwa taasisi kama FADev kuweza kusajiliwa na kufanya kazi. Mabadiliko yaliyofanywa na Serikali kwenye sekta ya madini yamewezesha sekta ndogo ya uchimbaji mdogo wa madini kutambuliwa zaidi na kupewa msukumo mkubwa. Ni imani yetu kuwa ili Serikali iweze kutimiza malengo yake kwenye sekta hii na ili mafanikio yaliyopatikana yaweze kuwa endelevu, ushiriki wa taasisi zisizo za kiserikali kama FADev ni muhimu. Tunazidi kushukuru ushirikiano na uwezeshaji tunaoendele kuupata kutoka tassisi mbali mbali za Serkali na hasa Wizara ya Madini, Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Shirika la Madini la Taifa (STAMICO), Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na kamati ya Bunge ya Nishati na Madini.

Aidha, natoa shukurani zetu kwa Shirika SWISSAID Tanzania kwa ufadhili wao tangu hatua za awali za uanzishwaji wa FADev mpaka sasa. Nwpenda pia kuwashukuru walengwa wetu ambao ni wachimbaji wadogo wa madini na jamii inayowazunguka ambao wameweza kuipokea FADev na kuiona kama mbia muhimu katika harakati zao za kupambana na umaskini. Na mwisho, lakini siyo kwa umuhimu, naipongeza Sekretarieti ya FADev kwa kufanya kazi kwenye mazingira magumu na kupata mafanikio makubwa.

Kama ambavyo Rais wa awamu ya tano Hayati John Pombe Magufuli alivyokuwa akitukumbusha mara kwa mara, nchi yetu imejaliwa kuwa na utajiri wa aina mbali mbai za raslimali madini. Lakini, ili madini haya yaweze kuwanufaisha Watanzania wa kawaida, ni budi tassisi zisizo za kiserikali kama FADev ziweze kufanya kazi kwa karibu na Serikali ili kuwasaidia na kuwaendeleza wachimbaji wadogo kama ilivo kwenye sekta nyingine za kilimo, mifugo na uvuvi. Sisi tumedhamiria kuijenga FADev iwe taasisi imara, yenye weledi na mifumo inayokidhi matakwa ya kitaifa na kimataifa na itakayofanya kazi kwa karibu na Serikali na Taasisi za kimataifa kuendeleza uchimbaji mdogo wa madini.

Mara tu baada ya kusajiliwa na kupata vibali vyote vinavotakiwa ili kufanya kazi kisheria hapa Tanzania, Baraza la Uongozi limeweka msisitizo mkubwa kwenye kujenga na kuimarisha misingi ya kuendesha FADev. Tumefanya mikutano mikuu ya mwaka ya wanachama miwili kama katiba yetu inavyotaka. Maazimio ya mikutano hii yametekelezwa. Baraza la Uongozi ambalo ndicho chombo kikuu cha kusimamia shughuliza kila siku za FADev limefanya jumla ya vikao vitatu kwa mujibu wa katiba na limeisimamia sekretariati katika kazi zake za kila siku. Baraza la uongozi limeandaa na kuweka mifumo na miongozo ya kitaasisi ya kusimamia raslimali za FADev ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa FADEv inajisajili kwenye mamlaka zinazotakiwa kisheria kama Mamlaka ya Mapato Tanzania, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii, Bodi ya Mikopo ya wanafunzi wa Elimu ya Juu, na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi.

Aidha, tumeandaa Mpango Mkakati (Strategic Plan) wa miaka mitano (2020-2025) ambao utaongoza mwelekeo wa FADev katika kipindi hiki. Katika uchanga wetu, tayari tumeanza kutekekeleza miradi mbalimbali kwa wachimbaji wadogo kama ilivuoainishwa kwa kina katika ripoti hii na kwenye utangulizi wa Katibu Mtendaji.

Pamoja na mafanikio tuliyoyapata, tunatambua changamoto ambazo zinatukabili. Tumeziainisha kwa kina kwenye Mpango Mkakati wetu. Hapa naomba niongelee changamoto moja kubwa; ya kutegemea mfadhili mmoja, Swissaid. Tumejizatiti kukabiliana na changamoto hii na tayari tumebaini wadau wa maendeleo mbao tunaweza kufanya kazi nao na tunaandaa mkutano nao ambao utafanyika kabla ya mwezi Juni mwaka huu.

Tayari taasisi mbalimali zikiwemo tassisi za kifedha, mashirika ya kimataifa na makampuni makubwa ya uchimbaji madini hapa nchini yameonyesha nua ya kufanya kazi pamoja na FADev.

Safari yetu ndiyo kwanza inaanza. Tunaamini msemo maarufu usemao "Ukitaka kwenda haraka, nenda peke yako; ukitaka kwenda mbali, nenda na wenzio". Tuna nia ya kwenda mbali, karibu ujiunge na sisi ili twende pamoja.

**John-Bosco Tindyebwa**
**Mwenyekiti, Baraza la Uongozi la FADev**

## Ujumbe kutoka kwa Katibu Mtendaji



Imekuwa safari iliyoje kwetu!
Hadi wakati huu ninapoandika ujumbe huu ambao ni wa kwanza kabisa kwenda kwa umma, kutoka kwenye shirika pekee ambalo shughuli zake zinalenga kuimarisha sekta ya uchimbaji mdogo, inaburudisha na kuleta hofu kwa wakati mmoja, ukizingatia kazi iliyopo mbele.

Ilikuwa mnamo Juni 2018 ambapo timu ya wataalamu wawili iliombwa kuratibu kazi juu ya masuala ya Uchimbaji Mdogo wa Madini ambayo ilishughulikiwa kwa pamoja na ushirikiano wa wataalam, ambao wakati huo ulijulikana kama Kikundi cha Kujifunza na Uongozi.

Leo, ninapowasilisha ujumbe huu kwako, Taasisi ya Kuendeleza Uchimbaji Mdogo (FADev) imepitia mageuzi na mapendekezo ya majina kadhaa ambayo yamekuwa yakibadilika mara kwa mara. Moja ya majina lilitotumika kwa muda mrefu katika historia ya shirika hili ni Jukwaa la Majadiliano ya Kuendeleza Uchimbaji Mdogo Tanzania (JUMKUTA)! Ninapata msisimko mkubwa ninapolitaja jina hili.

Kwa mtazamo zaidi, tuko katika karne ya 21 lakini taswira ya Sekta ya Uchimbaji Mdogo wa Madini nchini Tanzania bado linaonesha hii ni moja ya sekta ambayo haina mpangilio mzuri ikiwa hali inayopelekea kuonekana kuwa na shughuli ambazo zina madhara makubwa kwenye afya ya wachimbaji na jamii zao, shughuli zisizo salama na zisizo rafiki katika mazingira.

Taswira hii isiyopendeza inaendelea kushika kasi wakati ambapo kuna matokeo chanya na mazuri zinazohusianishwa na shughuli za Uchimbaji Mdogo wa Madini, na matokeo haya chanya hayazungumziwi na wala hayazingatiwi sana kwa kuwa hakuna wa kuyaibua. Dhana hii imekuwa kwa kiwango kikubwa kutokana na uhaba wa vielelezo na ushahidi kuhusu juhudi ambazo zimefanyika kubadilisha mtazamo huu hasi juu ya sekta ya Uchimbaji Mdogo wa Madini.

Wakati wa kuanzishwa kwa kile ambacho leo ni Taasisi ya Kuendeleza Uchimbaji Mdogo (FADev), utafiti ulifanyika ili kutoa taarifa juu ya umuhimu na mafanikio ya shughuli za kisekta za Uchimbaji Mdogo wa Madini, na pia kuangazia changamoto zinazoikabili sekta yenyewe. Hii ilifungua mlango na ulikaribisha fursa ya mdahalo wa kitaifa (Tanzania) yaliyofanyika

mnamo Novemba 2017. Wakati wa mdahalo washikadau husika walijadili na kuibua nguzo 5 zinazoweza kutekelezeka na Mwongozo wa njia ya mageuzi ya Sekta ya Uchimbaji Mdogo wa Madini Tanzania.

Mwaka 2019 ilidhihirika na kuafikiwa kuwa ili vipengele vya Mwongozo vitekelezwe kikamilifu, ni lazima kuwe na Shirika lililosajiliwa kisheria na Mnamo Julai 2019, FADev ilianzishwa. Kama Shirika, tumedhamiria sekta ya Uchimbaji Mdogo wa Madini ambayo ni shirikishi, adilifu na endelevu kwa kushirikiana wadau mbalimbali.

Kwa kutambua maono hayo, na kwa kupitia timu ndogo ya watalaam wanne (4) inayojumuisha Katibu Mtendaji, Meneja wa Programu na Utafiti, Mtalaam wa muda wa Masuala ya Kifedha, Msaidizi wa Utawala na Afisa wa Mradi wa Jinsia, tunategemea kufanikisha utekelezaji wa nguzo za kimkakati ambazo ziliibuliwa kwenye mdahalo na kuainishwa kwenye Mwongozo.

Kuna mengi sana ambayo tunajivunia kama FADev na wadau wetu kuendelea kuwa nasi bega kwa bega. Ndani ya kipindi kilichoanza wakati usajili wa FADev hadi wakati huu ninapoandika ujumbe huu, tumefanikisha mengi, lakini yafuatayo ni moja kati ya hatua muhimu tulizopiga:

- Tumejinasibu na kuweka wazi umuhimu wetu katika Sekta ya Uchimbaji, kwa kujikita zaidi kwenye sekta ya Uchimbaji Mdogo wa Madini.
- Tumeanzisha na kuendeleza mahusiano ya kikazi na Wizara za Serikali zinazohusika, Mawakala na Taasisi husika za Serikali, pamoja na wadau wengine wakuu wa Sekta ya Uchimbaji Mdogo wa Madini.
- Tumeanzisha na kudumisha mahusiano thabiti ya kikazi na mamlaka ya Serikali za mitaa na mikoa.
- Tumeanzisha Migodi ya Mifano mitatu.
- Tumeanzisha mpango wa Vifaa vya Kumilikisha kwa Kukodisha katika Migodi mitatu ya Mifano.
- Tumeanzisha mahusiano mzuri wa kikazi na vyombo vya habari nchini Tanzania.
- Tumeweka wazi umuhimu wa FADev kwenye sekta ya Uchimbaji Mdogo wa Madini Kitaifa, Kikanda na Kimataifa, na haswa kama Asasi ya Kiraia iliyokubaliwa kuwa Waangalizi katika Mkutano wa Minamata juu Matumizi ya Zebaki.

- Tumeanzisha na kufanya Uzinduzi wa Mradi wa Jinsia unaoshughulika zaidi na miradi ya vikundi vya Wanawake wanaoshiriki shughuli za Uchimbaji Mdogo wa Madini na Jamii zao.
- Tumeanzisha mahusiano ya kikazi na shirika la Kimataifa ya Wanawake Wanasheria na Maendeleo Barani Afrika (WiLDAF).
- Tulifanikiwa kikamilifu kuitikia wito wa dharura juu ya janga la Virusi vya Uviko-19 kwenye jamii ya Wachimbaji Wadogo wa Madini, kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee, na Watoto tulitoa elimu na kukuza uelewa juu ya janga la Uviko-19 kwenye jamii ya Wachimbaji Wadogo wa Madini.
- Tumefanikiwa kuandaa rasimu ya kwanza ya Mpango Mkakati wa Shirika

...na mengine mengi ambayo sitaweza kuyataja kweye ujumbe wangu.

Tuna nia ya dhati na uchu zaidi katika kufanikisha jukumu letu. Ili kuweza kufanya hivyo, kila mchango ni muhimu. Kwa hiyo unaposoma ujumbe huu, jumuika nasi katika ulimwengu huo ambapo sekta hii kubwa ya kiuchumi bado umelala, lakini tunaweza kwa pamoja kuisaidia sekta hii kufikia mafanikio makubwa na mahali pazuri kiuchumi. Hii inaweza kufanyika endapo tu sekta hii itapata uungwaji kamili kutoka Serikalini, kutoka kwa watunga Sera na wadau wanaovutiwa na sekta hii.

Binafsi, ninaloweza kujivunia katika kazi yangu ni kufanya kazi na timu ndogo lakini iliyojitolea, timu iliyohamasika kuchangia kwenye shughuli zinazolenga kuboresha maisha ya jamii za Wachimbaji Wadogo wa Madini. Hasa, ninafurahi kwamba wanawake kwenye sekta ya Uchimbaji Mdogo wa Madini ni kiungo muhimu kwenye shughuli za programu zetu.
Nina furaha na ninajivunia kuwa sehemu ya timu ya Shirika ambalo linajitahidi kuifanya sekta ya Uchimbaji Mdogo Wa Madini kuwa adilifu, shirikishi na endelevu.

Tafadhali, unaposoma ripoti hii, nakusihi ujikite kwenye kutafuta njia ambazo unaweza kushirikiana nasi kufanikisha ndoto hii!

Asante!
Ms. Theonestina Mwasha
**Katibu Mtendaji**

## Yaliyomo

Ujumbe kutoka kwa Mwenyekiti....i

Ujumbe kutoka kwa Katibu Mtendaji....iv

FADev ni akina nani?....1

Dira Yetu....1

Dhamira Yetu....1

Maadili Yetu....1

Nadharia Yetu ya Mabadiliko....1

Jinsi tulivyoanza....2

Kujenga Muktadha....2

Utafiti wa Awali....3

Ushiriki wa Mjadala wa awali....3

Mijadala ya Mada husika....3

Mjadala wa Kitaifa wa Kuchukua Hatua kuhusu Uchimbaji Mdogo....4

Mkakati wa Mageuzi ya Uchimbaji Mdogo....4

Machapisho....5

Katiba ya FADev....6

Muundo wa Uongozi wa FADev....6

Muundo wa Sasa wa Utawala....7

Baraza la Uongozi....7

Kamati ya Ushauri wa Kiutaalamu....8

Sekretarieti....9

Maendeleo na Mafanikio .......... 13
Ujengaji Uwezo na Uhamishaji wa Maarifa .......... 14
Upatikajani wa Mitambo: Mfumo wa Kukodisha na Kumiliki .......... 15
Utafiti na Kuendeleza Mijadala kati ya Wadau .......... 15
Kitovu cha taarifa za sekta ya uchimbaji mdogo .......... 19
Ushirikishwaji wa Vyombo vya Habari .......... 19
Mradi wa Jinsia .......... 21
Mwitikio wa Dharura Dhidi ya Janga la Uviko-19 .......... 24
Kujenga Uelewa Kwenye Eneo la Kazi .......... 28
Stadi za maisha: Mafunzo ya kutengeneza sabuni .......... 30
Mafanikio Makuu .......... 32
Changamoto Kuu .......... 34
Vyanzo vya Mapato vya Sasa: .......... 34
Mahitaji na Vyanzo vya Fedha Vilivyopo: .......... 35
Athari za Kutokuwa na Ufadhili: .......... 36
Matarajio na vipaumbele kwa miaka mitano ijayo .......... 37




## FADev ni akina nani?

Taasisi ya Kuendeleza Uchimbaji Mdogo (FADev) ni Shirika lisilo la kiserikali lililosajiliwa mwezi Julai mwaka 2019, katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya Sheria ya Mashirika yasiyo ya Kiserikali ya mwaka 2002, kwa usajili Na. 00NGO/R/0251. Makao makuu ya Taasisi yako Dar es Salaam.

| Dira Yetu | Maadili Yetu | Madili Yetu |
|---|---|---|
| Kuwa na sekta ya uchimbaji mdogo unaowajibika, shirikishi na endelevu. | Kukuza uchimbaji mdogo wa madini unaowajibika na endelevu, kupitia uwezeshaji, ushirikishwaji na mabadiliko ya sera. | • Uadilifu<br>• Uwajibikaji<br>• Usawa<br>• Ushirikishwaji<br>• Kushirikishana maarifa |

**Nadharia Yetu ya Mabadiliko**

WEZESHA → JENGA UHUSIANO → MAGEUZI



## Jinsi tulivyoanza

Uanzishwaji wa FADev ulitokana na michakato ya kujenga mawanda ya muktadha, utafiti wa awali, kuhusisha mijadala tofauti ya awali, mjadala iliyojengwa kwenye mada husika pamoja na mijadala ya kitaifa. Michakato hii ilithibitisha hitaji la kuwa na shirika ambalo shughuli zake zitajikita katika mnyororo wa thamani wa Sekta ya Uchimbaji Mdogo.

### Kujenga Muktadha

Kufuatia kushiriki katika mjadala wa uchimbaji mdogo uliofanyika nchini Ghana kwa kuwezeshwa na Taasisi ya Kimataifa ya Mazingira na Maendeleo (IIED), shirika la HakiMadini (shirika la Tanzania linalofanya kazi katika sekta ya madini) liliandaa hati ya usuli kuhusu uchimbaji mdogo wa Tanzania. Baada ya hapo, shirika la HakiMadini kwa kushirikiana na IIED waliandaa ziara za mafunzo na kupata uzoefu zilizofanyika Arusha na Dar es Salaam mwezi September 2016. Lengo la ziara hizi lilikuwa kuihusisha serikali, jumuiya ya wachimbaji wa madini na mashirika ya kiraia ili kuwa na uelewa juu ya muktadha wa jumla kuhusiana na sera ya uchimbaji mdogo, desturi na dhana zilizopo.

### Utafiti wa Awali



Ziara ya kupata uzoefu ilifuatiwa na utafiti ambao ungekuwa msingi wa mjadala. Kwa kufuata mchakato wa zabuni, kampuni ya MTL Consulting iliyopo jijini Dar es Salaam ilifanya utafiti wa awali ambao ulitoa Mwongozo kwenye mjadala. Watafiti walirekodi ushahidi kuhusu uchimbaji mdogo nchini Tanzania kwa kupitia utafiti wa awali, na mapitio ya machapisho na matokeo yalipitiwa na Kamati ya Utafiti na Ushahidi ili kuhakikisha ufaafu, uthibitishaji wa ukweli na ubora wa utafiti. Wadau wa uchimbaji mdogo walioombwa ushauri ni pamoja na, wamiliki wa Leseni ya Uchimbaji, jamii za wachimbaji, vyama vya wachimbaji wadogo ikiwa ni pamoja na vikundi vya wanawake, watoa huduma, mashirika ya kiraia, mashirika ya serikali katika ngazi za mkoa, wilaya na kijiji yanayojihusisha na uchimbaji wa madini na sekta zinazohusu madini, vyombo vya habari na wanataaluma.

### Ushiriki wa Mjadala wa awali

Kwa kufuata mchakato wa zabuni, shirika la HakiMadini liliteuliwa kuwa Mwendesha Mjadala na kwa kushirikiana na IIED na MTL Consulting waliendesha mijadala iliyohusisha wadau wa sekta ya uchimbaji mdogo mnamo mwezi Mei 2017 huko Mirerani, Geita, Dodoma na Dar es Salaam. Katika mijadala hiyo, matokeo kutoka katika utafiti wa awali yalitolewa; vile vile washiriki walibainisha changamoto kuu, vipaumbele na yale yanayoweza kuwa masulushisho na walitoa maoni kuhusu uandaaji wa mjadala.

### Mijadala ya Mada husika

Taasisi ya Kimataifa ya Mazingira na Maendeleo (IIED) kwa kushirikiana na HakiRasilimali (jukwaa la hapa nchini la mashirika ya kiraia yanayojihusisha na sekta ya uziduaji), walifanya mfululizo wa mijadala iliyojengwa kwenye mada ndogondogo huko Arusha na Mwanza mwezi Septemba 2017. Mijadala hii iliwahusisha wachimbaji, watendaji wa ugavi na minyororo ya thamani, jumuiya ya wachimbaji, mashirika ya uchimbaji, vyama vya wafanyakazi,

chama cha wanawake, wanataaluma, mashirika ya kiraia na maofisa wa serikali wa ngazi ya kata. Mijadala iliyojengwa kwenye mada ndogondogo ilisaidia kubainisha masuluhisho yanayotekelezeka, kukiwa na wajibu na majukumu dhahiri yanayofanywa na wadau kadhaa katika sekta hiyo. Utafiti wa usuli, mfululizo wa mijadala ya wadau na mijadala iliyojikita kwenye mada ndogondogo kwa pamoja iliunda jumla ya maarifa kabla ya mjadala ambayo yalikuwa msingi wa Mjadala wa Kitaifa wa Uchimbaji Mdogo.

## Mjadala wa Kitaifa wa Kuchukua Hatua kuhusu Uchimbaji Mdogo

IIED kwa kushirikiana na HakiMadini, MTL Consulting, Kituo cha Kimataifa cha Utafiti wa Misitu (CIFOR) na COWI waliandaa tukio la mjadala wa kitaifa kuhusu uchimbaji mdogo lililofanyika mjini Geita, Tanzania kuanzia Novemba 7 - 10, 2017. Mjadala huu ulifunguliwa rasmi na Mkuu wa Mkoa wa Geita. Karibu wawakilishi 90 wa vikundi vya wadau mbalimbali walishiriki katika tukio hilo ambalo lilianza kwa ziara ya siku mbili ya kutembelea maeneo ya uchimbaji mdogo wa dhahabu ili kujifunza na kupata uzoefu. Hatua hii ilifuatiwa na mjadala rasmi kwa mfumo wa warsha ya siku mbili iliyolenga kutafuta suluhisho. Kwa kuzingatia masuluhisho yaliyopendekezwa kutoka katika shughuli zilizofanywa kabla ya mjadala, washiriki walifanyia kazi na wakabainisha hatua za kuchukuliwa haraka kwa kila moja wapo kati ya 'nguzo tano za suluhisho', zinazojulikana kama ardhi na leseni; biashara; mazingira, afya na usalama; masoko; na wanawake katika uchimbaji mdogo.

## Mkakati wa Mageuzi ya Uchimbaji Mdogo

Wadau wa uchimbaji mdogo nchini Tanzania waliokutana katika mjadala wa kitaifa ulifanyika mwezi Novemba 2017, walipata vipengele muhimu vya Mkakati huu chini ya 'nguzo tano za suluhisho' ambavyo ndivyo msingi wa Mkakati huu wa mageuzi ya Uchimbaji Mdogo nchini Tanzania. Hatua hizi ziliratibiwa kwa kuwa mageuzi yalipaswa kushughulikia mapengo yaliyopo katika sera na sheria, maarifa na utafiti, mawasiliano, uhusishwaji, uwezo na rasilimali.

Mkakati huu ulinufaishwa na shughuli mbalimbali zilizowakutanisha watu na mjadala uliofanywa na washiriki 90. Washiriki hawa walijumuisha wachimbaji na vyama vya wachimbaji ikiwa ni pamoja na makundi ya wanawake; maafisa wa serikali; wawakilishi kutoka katika makampuni makubwa ya madini; mashirika ya kiraia, taasisi za kitaaluma na mafunzo; vyombo vya habari, wachimbaji kutoka Uganda ma Kenya; na wageni kutoka Ghana, Zimbabwe, Uswisi na Marekani. Washiriki wa mjadala walifanyia kazi na kubainisha hatua za kuchukuliwa haraka kwa kila 'nguzo tano za suluhisho' zinazojumuisha ardhi na

leseni; uchimbaji mdogo, biashara iliyoimarika na yenye muunganiko, mazingira, afya na usalama; masoko; na wanawake katika uchimbaji mdogo.

Hatua zilizobaianishwa ziliratibiwa kwa kuwa mageuzi yalipaswa kushughulikia mapengo yaliyopo katika sera na sheria, maarifa na utafiti, mawasiliano na uhusishwaji; uwezo na rasilimali.

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **DIRA** | **SEKTA ADILIFU, SHIRIKISHI, NA ENDELEVU** | | | | |
| **MALENGO** | Sekta Rasmi na Halali Kisheria | Sekta inayojali Mazingira na Adilifu | Ushiriki wa Wanawake wenye tija Katika Sekta | Biashara Endelevu ndani na nje ya Sekta | Mijadala Shirikishi na Taasisi imara |
| Shughuli 1 | Maboresho ya sera na Urasimishwaji | Anzisha Programu ya Mazingira, Afya na Usalama | Utambuzi wa Wanawake Kisera na Taratibu | Migodi ya Majaribio | Kuanzisha na Kuendeleza Jukwaa la Majadiliano |
| Shughuli 2 | Kuwa na kituo cha taarifa za Kijiolojia | Kuhamasisha urekebishaji wa mazingira | Kuwa na Kituo cha majaribio kinachoongozwa na wanawake | Kuchangia uimarishwaji wa vituo vya umahiri | Kuwezesha vyama vya wachimbaji |

Nguzo zilizoainishwa hapo juu zinaunda sehemu ya vipengele muhimu vilivyopendekezwa kuwa sehemu ya mkakati wa mageuzi ya uchimbaji mdogo nchini Tanzania. Pia, mikondo mitano ya kazi inayojumuisha shughuli za msingi ilibainishwa kuwa ni kipaumbele kwa ajili ya utekelezaji kama ilivyooneshwa kwenye jedwali hapo juu.

## Machapisho



Ripoti za Utafiti, ripoti zinazotokana na shughuli za mijadala na michakato ya mijadala iliyopelekea kuanziswha kwa Taasisi ya FADev ianzishwe zinaweza kupatikana na kupakuliwa kwenye tovuti yetu kwa kufuata kisimbo hiki: www.fadev.or.tz.




## Katiba ya FADev

Katiba ya FADev imepewa mamlaka, wajibu na majukumu ambayo yameelezewa waziwazi. Licha ya miundo ya utawala ya shirika iliyopo sasa, utendaji na mamlaka, utamaduni mzuri ambao unathamini mashauriano na ushiriki wa wote utadumishwa.


### Muundo wa Uongozi wa FADev

Muundo wa uongozi wa FADev umeundwa kwa makusudi ili kuhakikisha ufanyaji wa maamuzi wenye ufanisi ili kufanikiwa kufikia dira, dhima na malengo ya Shirika. Hii ndiyo njia pekee, shirika litashikilia na kuhimiza uwajibikaji wa michakato endelevu.

Michakato ndani ya muundo wa Shirika inaendeshwa na maadili yake ya msingi ambayo ni:

1. Uhuru
2. Ushiriki
3. Uadilifu, na
4. Uwajibikaji.

## Muundo wa Sasa wa Utawala




## Baraza la Uongozi

Baraza la Uongozi linasimamia shughuli za FADev, Sekretarieti yake na hutoa mwongozo kuhusiana na Sera, bajeti na vipengele vingine vikubwa vya FADev na utekelezaji wake na wajibu wa Baraza la Uongozi hujumuisha:

a) Kuweka muundo na shughuli za Sekretarieti inayoongozwa na Katibu Mkuu
b) Kuunda Kanuni na Sheria kwa ajili ya usimamizi mzuri wa wafanyakazi, utawala, nyenzo na fedha za FADev
c) Kulinda na kuimarisha sifa nzuri ya Shirika
d) Kuajiri wajumbe waandamizi wa Sekretarieti na kuanzisha nafasi za kazi
e) Kushiriki katika kutengeneza Mipango Mkakati ya Taasisisi

f) Kumteua Mkaguzi wa mahesabu

g) Kujadili na kupitisha bajeti za mwaka kwa ajili ya kupewa idhini ya mwisho na Mkutano Mkuu

h) Kujadili na kuidhinisha mikutano, ripoti za utekelezaji halisi na masuala ya fedha

i) Kuunda kamati mbalimbali na kuanzisha matawi ya Shirika pale ambapo ni lazima.

### Kamati ya Ushauri wa Kiutaalamu

Kufuatia mchakato mrefu wa mashauriano wakati wa hatua za mwanzo, kabla ya mjadala na baada ya mjadala, jopo la wataalamu kwenye sekta ya uchimbaji mdogo linalojulikana kama kamati ya Ushauri wa Kitaalamu, iliyojulikana hapo mwanzo kama Jopo la Uongozi na Mafunzo, iliundwa ili kuyawakilisha makundi muhimu ya wadau wa uchimbaji mdogo na kuongoza mchakato wa 'utekelezaji' baada ya tukio la mijadala.

Jopo hili la wataalamu katika muktadha wa uchimbaji mdogo sasa wanatambulika kama kamati inayotegemewa kwa ushauri katika shirika. Kamati ya Ushauri wa Kitaalamu inaishauri Sekretarieti na Baraza la Uongozi kuhusu uandaaji wa Mkakati na mchakato wa utekelezaji na kutumia ushawishi wao binafsi na wa kitaasisi na wa watu ili kufanikisha masuluhisho ya mageuzi ya uchimbaji mdogo katika mjadala wa kitaifa.

Muundo wa Kamati ya Ushauri wa Kiufundi hujumuisha wanakamati wanaowakilisha mashirika ya kiraia na wawakilishi kutoka katika wizara na idara husika za Serikali. Wawakilishi kutoka Serikalini wanakaa katika kamati ya Ushauri wa Kitaalamu kama waangalizi, kama ilivyoonyeshwa katika jedwali hapa chini.

| WANACHAMA HAI | |
|---|---|
| Jina | **Shirika** |
| Bi. Salma Kundi | Mwenyekiti – Kamati ya Ushauri wa Kiufundi<br>Chama cha Wachimbaji Wanawake wa Tanzania (TAWOMA) |
| Dkt. Curtis Msosa | Makamu Mwenyekiti – Kamati ya Ushauri wa Kiufundi<br>Mchimbaji binafsi |
| Bw. Haroun Kinega | Shirikisho la Vyama vya Wachimbaji wa Tanzania (FEMATA) na REMA |

| | |
|---|---|
| Bw. Salum Mkango | Taasisi ya Utafiti wa Madini (MRI),<br>Taasisi za kitaaluma na mafunzo |
| **WAANGALIZI** | |
| Bw. Francis Mihayo | Wizara ya Madini<br>- Kamishina Msaidizi - Uchimbaji Mdogo |
| Bw. Leo Mavika | TAMISEMI<br>- Kiongozi, Uratibu wa Kisekta |
| Bi. Glory Kombe | NEMC<br>Meneja, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini |
| Bw. David Malissa | Wizara ya Ardhi, Nyumba na Makazi<br>- Afisa Ardhi Mwandamizi |

## Sekretarieti

FADev inafanya kazi kama Shirika binafsi Lisilo la Kiserikali linalowahusisha wadau wengi likifanya kazi chini ya usimamizi wa moja kwa moja wa Baraza la Uongozi ili kutekeleza shughuli zake za msingi bila kujihusisha au kuingiliwa na siasa kwa namna yoyote ile. Hata hivyo, katika shughuli zake zote, FADev inasaidia utekelezaji wa malengo ya kisekta ya Serikali kwa kutoa ushauri wa kitaalam na wa kisera kadiri inavyohitajika.

Itakapokuwa na uwezo wa kifedha na kitaasisi, FADev inalenga kutenda kazi kama shirika lenye mafanikio ambalo linakusanya na kuoanisha taarifa mbalimbali, kuratibu mijadala, kutekeleza wajibu wa kuwa kituo cha mawasiliano kuhusu masuala yanayohusiana na uchimbaji mdogo, kujenga ushirikiano na kutekeleza vipengele vyake vya kimkakati kwa kuzingatia mikondo ya kazi iliyopo kwa namna ifuatayo:

### *Kuratibu uundwaji na utekelezaji wa Mkakati wa mikondo ya kazi*

Kama kipaumbele, sekretarieti ya FADev inaratibu, chini ya usimamizi wa Baraza la uongozi, na ushauri kutoka katika Kamati ya Ushauri wa Kitaalam pamoja na washirika kuhusu utekelezaji wa nguzo hizo tano za kimkakati, ambazo ni:

i. **Kuhimiza shughuli za uchimbaji mdogo ambazo ni halali na rasmi nchini Tanzania**

Kurasimisha na kuhalalisha sekta ya uchimbaji mdogo huhitaji mageuzi katika sera na miongozo ya kisheria iliyopo, uhusikaji wa wadau wengi na kujenga uelewa kupitia mawasiliano ya kiubunifu na programu za mafunzo. Pia inahitajika mifumo ya usaidizi inayolenga kutoa ardhi iliyopimwa, takwimu za kijiolojia, huduma za ushauri kwa wachimbaji wadogo na motisha katika kufanikiwa kuwa na shughuli za uchimbaji ambazo ni rasmi na halali.

*FADev hufanya kazi pamoja na wadau wengine katika kufanya mageuzi ya sera kuhusiana na ardhi na leseni za madini. Kama sehemu ya kuanzia, mchakato huu unahakikisha kwamba kunakuwa na fasili ya wazi ya istilahi zinazotumika kuelezea sekta hii na tofuati za viwango mbalimbali vya utendaji kazi, hasa katika uchimbaji mdogo wa madini.*

ii. **Kuhumiza uchimbaji mdogo unaojali mazingira na jamii**

Mageuzi yanayolenga kuboresha utendaji wa kimazingira na kijamii wa sekta ya uchimbaji mdogo yanapaswa kupata motisha kutokana na sababu za biashara kwenye sekta ya uchimbaji mdogo na uwezo wa kuhamasisha uchumi wa kijani. Mara nyingi, uingiliaji kati unaosababishwa na hitaji la kuchukua hatua 'kukomesha' 'madhara' ya kimazingira na kijamii yanayosababishwa na shughuli za sekta hii. Hii imeonesha haina manufaa. Kwa kuwa katika mazingira mengi, shughuli za uchimbaji mdogo zinafanywa ili kukabiliana na umasikini, kwa makusudi haya mafanikio ya sekta hii yanakuwa mashakani. Hata hivyo, ikiwa shughuli za uchimbaji mdogo zitasimamiwa vizuri, zinaweza kuwa chanzo kikuu cha maendeleo ya kiuchumi kwa familia na jamii ya wachimbaji wadogo kwa ujumla.

*FADev tayari imekwishaanzisha kipengele cha programu ya Mazingira, Afya na Usalama ambacho kinajumuisha shughuli kadhaa ambazo zinahamasisha desturi za uchimbaji mdogo zinazozingatia afya, usalama na utunzaji wa mazingira.*

iii. **Kuhamasisha Ushiriki wa Wanawake katika Uchimbaji Mdogo**

Michakato ya mageuzi inayolenga kuwawezesha wanawake katika uchimbaji mdogo inapaswa kuzingatia masuluhisho yanayogusa masuala ya kijamii, kisheria,

kiuchumi, kiufundi, kitaaluma na kisiasa. Masuluhisho hayapaswi kutafutwa kwa sababu tu ya kushughulikia vikwazo ambavyo wanawake katika uchimbaji wa madini wanakabiliana navyo bali yanapaswa kutambua na kujenga juu ya uwezo wao ili kuweza kuongeza thamani muhimu katika uchumi, biashara, ufanyaji wa maamuzi, na namna bora ya kufanya kazi.

*Katika shughuli zake za programu, FADev ufanya kazi kushughulikia mapengo ya kijinsia katika sera na sheria ya uchimbaji madini ambayo inatambua kikamilifu wajibu na haki za wanawake ndani ya sekta ndogo – si tu jinsia kwa ujumla wake. FADev pia ina kipengele cha mradi ambacho kinalenga kuanzisha na kuimarisha vyama/mashirika yanayoongozwa na wanawake ili kuonesha na kuweka mfano mzuri kwa ajili ya sera iliyobadilishwa na kuwahamasisha wanawake wengine wenye uwezo.*

iv. **Kusaidia Maendeleo ya Biashara Endelevu yenye Tija ndani na nje ya sekta ya Uchimbaji Mdogo**

Kutokana na uwezekano wa mafanikio kwa watendaji wa sekta ya uchimbaji mdogo kama wajasiriamali wenye uwezo, usaidizi mahususi katika maeneo kama vile fedha, masoko, ujuzi wa kitaalam na teknolojia, stadi za biashara na uongozi huweza kuwa muhimu katika kupata thamani ya kiuchumi kwenye sekta. Umuhimu wa mpango wa biashara wa muda mrefu unapaswa kuhimizwa ili kuwaandaa wachimbaji kwa ajili ya fursa kupanuka zaidi katika biashara endelevu zisizokuwa za uchimbaji wa madini.

*FADev ufanya kazi na wamiliki wa leseni za uchimbaji mdogo ili kutengeneza na kuanzisha Migodi ya Mfano ya Uchimbaji Mdogo kama njia ya kutimiza desturi bora za uchimbaji wa madini na biashara. Migodi ya Mfano ya Uchimbaji Mdogo ni hatua muhimu katika kuonesha na kuweka mfano mzuri wa biashara za uchimbaji mdogo zinazofanywa kwa kuwajibika na zenye mafanikio ambazo zinachangia maendeleo ya sehemu husika kupitia uongezaji wa thamani, ajira na kodi. FADev hutoa tathmini ya kina na mwongozo kuhusu vituo vya mafanikio vya Migodi ya Mfano ya Uchimbaji Mdogo.*

v. **Mijadala Jumuishi na Utafiti**

Kufuatia mjadala wa kitaifa wa uchimbaji mdogo, uwezeshaji wa mijadala ya kitaifa na kimataifa, utabaki kuwa alama ya biashara ya FADev. Hili linabaki kuwa suala

muhimu katika uhimizaji wa mafunzo yanayohusisha sekta mbalimbali, kushirikishana maarifa/uzoefu na ushirikiano ili kufanikiwa kuwa na sekta ya uchimbaji mdogo inayowajibika, jumuishi na endelevu.

> *FADev inaandaa jukwaa la kisasa na la kiubunifu kwa ajili ya kuwaunganisha wadau wengi wa Tanzania wa sekta ya uchimbaji mdogo kama njia ya kuhamasisha mawasiliano endelevu baina ya wadau wa sekta ya uchimbaji mdogo ndani na nje Tanzania, na usambazaji wa taarifa kwa kutumia teknolojia ya kisasa. Jukwaa hili litatumika kama kituo cha taarifa kukusanya pamoja taarifa husika za uchimbaji mdogo ili wadau waweze kuzipata kwa urahisi.*

Sekretarieti, kwa kuwabainisha washirika husika wa utekelezaji kwa kila mkondo wa kazi na kupata bajeti, FADev na washirika husika wataendelea na utaratibu sahihi wa kimkataba ili kufanya shughuli za utekelezaji na ufuatiliaji.



## Maendeleo na Mafanikio

Simulizi inabadilika. Kulingana na utayari wa serikali kufanya kazi na wadau wa sekta ya uchimbaji mdogo na uwepo wa FADev na vyama vingine vya wachimbaji, kuna nuru inayoonekana kwa mbali.

Kihistoria, taswira maarufu iliyojengwa kuhusu sekta ya uchimbaji mdogo ni ile inayoonesha kwamba ni sekta chafuzi na isiyojali utunzaji wa mazingira, wala jamii kwenye maeneo inamoendesha shughuli zake.

Katika mchakato wa kurasimisha na kuhalalisha sekta ya uchimbaji mdogo, ambalo ni hitaji la sasa, ni Dhahiri kuwepo na uhitaji wa maboresho kwenye sera na miongozo ya kisheria iliyopo. Hii inaweza kufanywa tu kupitia ushiriki wa sekta nyingi na kujenga uelewa kwa kutumia mawasiliano ya kiubunifu na programu za mafunzo.

FADev imeanzisha masuluhisho yanayotekelezeka katika muktadha wa uchimbaji mdogo, ambayo ni ya kimfumo, ya wazi na shirikishi. Masuluhisho haya yanajumuishwa katika utekelezaji wa shughuli katika maeneo yafuatayo, ambayo yamekubaliwa na wadau hasa wachimbaji wadogo wa madini.

## Ujengaji Uwezo na Uhamishaji wa Maarifa



Mazingira ya uchimbaji mdogo uendeshwa kwa kutumia uzoefu wa waasisi wa shughuli za uchimbaji mdogo wa madini. Hii humaanisha, kuna ukosefu wa maarifa ya kuendesha sekta hii kama biashara.

Kama sehemu ya kuanzia, mkazo wa FADev umekuwa kwenye kuleta mtazamo mpya miongoni mwa wachimbaji. Mtazamo huu mpya umeonekana kuwa muhimu sana, na wachimbaji wanaonekana kujuta kwa nini FADev haikuanzishwa mapema.

Katika kipengele hiki, tumejikita kwenye, na kulingana na matokeo ya uchanganuzi wa pengo:

- Kutengeneza moduli/mtaala wa mafunzo mahususi kwa ajili ya kila kundi lengwa.
- Kutoa mafunzo kwa vituo 3 vya FADev vya Migodi ya Mfano ya Uchimbaji Mdogo kuhusu uzingatiaji wa kisheria, kazi yenye staha, uwajibikaji wa sijamii, uwajibikaji wa kimazingira na jinsi ya kuongeza uzalishaji wao. Mafunzo haya pia hujumuisha:
  - ✓ kujenga uelewa miongoni mwa wachimbaji kuhusu mwongozo wa kisheria na kiusimamizi ndani ya muktadha wa Tanzania
  - ✓ kuwasaidia wachimbaji kuboresha hali za kiafya na usalama mahali pao pa kazi.
  - ✓ kuwasaidia wachimbaji ili kuhakikisha kwamba shughuli zao zinafanywa katika hali ya mazingira inayokubalika.
  - ✓ kuboresha uelewa wa kitaalam miongoni mwa wachimbaji ikiwa ni pamoja na njia salama ya uchenjuaji.

- ✓ kujenga uelewa kuhusu ajira za watoto na ulinzi kwa mtoto (hatari za kuwaajiri watoto kwenye migodi).
- ✓ kuboresha usawa wa kijinsia katika shughuli za uchimbaji mdogo wa madini na kwenye sekta kwa ujumla wake.
- ✓ kuboresha ujuzi wa kutatua migogoro kwa wachimbaji.

## Upatikajani wa Mitambo: Mfumo wa Kukodisha na Kumiliki

FADev inazingatia sana kuhakikisha kwamba wachimbaji hawaachwi nyuma wala hawachanganywi na matumizi ya teknolojia mpya katika muktadha wa uchakataji wa uchimbaji mdogo.

Ili kuhakikisha kwamba tunaanza na wachimbaji kutoka pale walipo, tumechukua hatua ya Maboresho zaidi. Hatua ambayo inatafuta kuboresha mifumo ya uzalishaji ya uchimbaji mdogo kuanzia pale walipo wachimbaji, na wadau wengine kwa kuzingatia uboreshwaji wa uelewa, ujuzi wa kitaalam na zana kwa jumla.

Hadi sasa FADev imetekeleza shughuli za kuboresha miundombinu na zana, ikiwa ni pamoja na:

- ✓ kuboresha mazingira ya kufanyia shughuli za uchimbaji mdogo, na
- ✓ kutoa na kufunga mitambo ya kuchimbia na kuchakata madini kwenye migodi husika, kwa kuzingatia mahitaji yaliyopo kwa sasa. FADev inatoa ruzuku kupitia mfumo wa kukodisha na hatimaye kumiliki vifaa hivyo. Wamiliki binafsi wa migodi wanayo nafasi ya kuchagua kushiriki katika mfumo mmoja au yote.

## Utafiti na Kuendeleza Mijadala kati ya Wadau

Pasipo sisi wenyewe kujipa sifa, hili ni tukio la kwanza na la aina yake kushughulikia masuala ya wadau na kutoa nafasi ya mjadala wa sera yanayohusiana na sekta ya uchimbaji mdogo ndani ya mipaka ya Tanzania.

Kwa kuzingatia historia yake, FADev inawakutanisha pamoja wadau wa sekta ya uchimbaji mdogo kwa kuweka mazingira yanayowajumuisha wadau ikiwemo mijadala shirikishi yenye taarifa muhimu.



Kikao cha kimkakati Dodoma_2018



Mdahalo ya Wadau wa Sekta Mwanza_2018



Elimu ya kujikinga dhidi ya Uviko-19, Nyarugusu_2020



Kikao cha wadau wa Sekta, Dar es Salaam_201



Ukusanyaji taarifa za awali, Ibondo_2019



Ziara ya Mafunzo, Nsangano_2019





19



Wanawake wachimbaji wadogo, Nyakagwe_2019









Elimu ya Usalama_2020

Moja wapo kati ya malengo makuu ya FADev ni kuwezesha kuongoza mijadala ya kitaifa, kikanda na kimataifa inayojikita katika shughuli za kisekta za uchimbaji mdogo.

Kwa kuwa ni shughuli kuu ya kipengele cha programu, mijadala ya sekta nyingi hubaki kuwa muhimu katika kuhimiza mafunzo shirikishi, kuonesha desturi bora zaidi za kufanya shughuli za uchimbaji mdogo, na kuimarisha ushirikiano ili kufanikiwa kuwa na sekta ya uchimbaji mdogo yenye kuwajibika, jumuishi na endelevu.

Tangu kusajiliwa kwake kama Shirika Lisilo la Kiserikali nchini Tanzania, shirika la FADev limefanya kazi na linaendelea kufanya kazi katika kuimarisha uhusiano wa kazi pamoja na wadau muhimu katika maeneo yao, kitaifa, barani Afrika na zaidi.

Ili kufanya jambo hili kwa ufanisi, FADev inawekeza, kadiri fedha inapopatikana, katika kuielewa sekta ya uchimbaji mdogo ndani Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hii imefanyika kupitia:

- ✓ kuanzisha mjadala uliojikita katika mada muhimu kisekta
- ✓ kufanya Kongamano ya Wadau wa Maendeleo – la kwanza lilifanyika mwaka 2019[1]
- ✓ kufanya kazi ya kubainisha shughuli za uchimbaji mdogo
- ✓ kufanya tafiti mbalimbali za kukusanya taarifa za awali
- ✓ kufanya tathmini ya mahitaji endelevu ya wachimbaji wadogo wanaoshirikiana na FADev
- ✓ kuendelea kuishirikisha Serikali kupitia Wizara husika kama vile:
    - i. Wizara ya Madini na wakala zake
    - ii. Ofisi ya Rais: Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI)
    - iii. Ofisi ya Makamu wa Rais: Muungano na Mazingira na wakala zeke, na
    - iv. Wizara ya Ardhi, Nyumba na Makazi
- ✓ kuendelea kuwahusisha watunga sera kupitia kamati husika za Bunge, hasa kamati ya Bunge ya nishati na madini

---

*1 Kwa sababu ya janga la ugonjwa wa virusi vya Uviko-19, mfululizo wa Tukio la Maendeleo ya Washirika hauwezi kufanyika mwaka 2020.*

Kwa ufupi, shughuli za utafiti na kuendeleza ushirikishwaji wa wadau mbalimbali ikiwemo kushirikishana uzoefu, ina hakikisha mtu yeyote, hususan wachimbaji wadogo, wasiachwe nyuma.

## Kitovu cha taarifa za sekta ya uchimbaji mdogo

Kazi ya kutengeneza jukwaa la kisasa la kibunifu ambalo litakuwa ni kichocheo cha ushiriki wa taarifa na uhusiano kati ya wadau wa sekta ya uchimbaji mdogo nchini Tanzania, inaendelea.

Kituo hiki cha kushirikisha uzoefu, kuwahusisha wadau wengi na kuwaunganisha wataalamu kimeanzishwa kwa makusudi ili kuhimiza uwasilishaji wa maarifa kwa wakati na kushiriki nyenzo za utafiti zinazozalishwa na FADev, washirika wake na wataalamu wa kimataifa ili kuhamashisha mageuzi ya sera na utendaji kazi katika sekta ya uchimbaji mdogo.

Wakati huo huo, jukwaa hili litatumika kama kituo cha taarifa kinachokusanya taarifa zote husika za uchimbaji mdogo kwa ajili ya kuwafikia wadau kwa urahisi, kushiriki maarifa na kujenga uelewa kuhusu njia bora zaidi ndani ya muktadha wa uchimbaji mdogo kimataifa.

## Ushirikishwaji wa Vyombo vya Habari



Sekta ya uchimbaji mdogo ni sekta ndogo ya kiuchumi inayoeleweka vibaya zaidi duniani! Kuna taarifa nyingi kuhusu sekta ya uchimbaji mdogo vile inavyoleta uharibifu, hasa katika mazingira.

Ingawa sekta hii ina faida nyingi, ikiwa ni pamoja na kuhudumia takriban wananchi 6,000,000 wanaoishi kwenye maeneo ya uchimbaji mdogo wa madini, vyombo vya habari siku zote vimekuwa vikiangazia masuala yanayohusu uchafuzi wa hewa na uharibifu wa mazingira tu.

Ripoti hizi zinatokana na, kwa kiwango kikubwa, kukosekana kwa elimu kwa upande wa waandishi wa habari kuhusu sekta ya uchimbaji mdogo.

FADev inachukua hatua ya makusudi kabisa kuwahamasisha na kuwahusisha watendaji wa vyombo vya habari, hasa, waandishi wa habari, katika michakato jumuishi ya mafunzo ambayo hujumuisha ziara za kwenda kwenye maeneo husika ya uchimbaji ili kukuza ufahamu na kuwapa fursa halisi ya kujionea wenyewe.

Mbinu hii imeimarisha mambo yafuatayo:

- ✓ ushirikiano imara wa kazi pamoja na vyombo vya habari
- ✓ ubainishaji wa maslahi ya kiuandishi wa habari ili kusaidia kuona ni aina gani ya ujengaji uwezo inahitajika miongoni mwa waandishi wa habari.
- ✓ kubainisha waandishi wa habari kupitia vyombo vya habari wanakofanyia kazi, ambao wataendelea kufanya kazi na FADev katika kuuelimisha umma na wadau wengine kuhusu masuala yanayohusiana na sekta ya uchimbaji mdogo.
- ✓ Uhamasishaji na kutoa elimu kwa umma kwa wingi juu ya sekta ya uchimbaji mdogo kupitia vyombo vya habari kwenye maeneo husika, Kitaifa na kimataifa.





## Mradi wa Jinsia

Kumekuwa na nia ya kimegeuzi katika sekta ya uchimbaji mdogo kwa miaka mitano iliyopita (2015 – 2020). Nia hiyo pia imeoneshwa na uongozi wa Serikali iliyokuwa madarakani, chini ya Uongozi wa hayati Ndg. John Pombe Magufuli.

Nia hii inatokana na uwezekano wa mafanikio ya kiuchumi kutokana na shughuli za sekta ya uchimbaji mdogo. Vilevile kile kinachoonekana ni udhihirisho wa uwezo kutokana na shughuli za sekta ya uchimbaji mdogo katika kukuza maendeleo vijijini, hasa katika jamii ambamo shughuli za uchimbaji mdogo zinafanyika.

Sera ya Kitaifa ya Madini ya mwaka 2009 inahimiza ushiriki wa wanawake katika shughuli za uchimbaji mdogo katika idara zake, kama vile: Uchimbaji mdogo wa dhahabu, uchimbaji wa madini ya vito na uchimbaji mkubwa wa madini. Hii inaweza kuchukuliwa kuwa ni hatua muhimu kwa ajili ya kuwahusisha wanawake katika sekta ya uziduaji kwa ujumla wake.

Sera za kitaifa na miradi mingine ya kimkakati inayofanywa na Serikali huwahimiza wanawake kushiriki katika shughuli za uchimbaji mdogo. Hata hivyo, wanawake katika sekta ya uchimbaji mdogo katika muktadha wa Tanzania, bado wapo katika nafasi za chini za uongozi na zile za kufanya maamuzi. Na wao, wanawake, ndio wanahangaishwa zaidi na hali ya umasikini kuliko wenzao ambao ni wanaume.

Hii pia inaweza kuonekana katika jitihada zilizofanywa na serikali ya awamu ya tano kupitia miradi ya kimkakati ya kuanzisha mfumo ambao unaruhusu Serikali kupitia Wizara ya Madini kuwa na Kongamano ya kila mwaka la kujadili sekta ya uchimbaji mdogo. Kupitia Wizara ya Madini, kumekuwa na mkutano wa kitaifa (Januari 2019), na mkutano wa kimataifa (Februari 2020) ukiwakutanisha pamoja wadau wa tasnia hii.

Ripoti zinaonesha kwamba idadi ya wanawake katika sekta ya uchimbaji mdogo ni asilimia 27[2] ya nguvu kazi yote ya sekta ya uchimbaji mdogo. Takwimu hizi zilizokadiriwa zinaweza kupingwa kwani ushiriki wa wanawake katika shughuli za uchimbaji mdogo huingiliana na sekta ya kilimo.

Katika uzinduzi wake wa Mradi wa Jinsia ulioanzishwa Desemba 2020, FADev inafanya jitihada chanya kuvunja kiza kilichowakumba wachimbaji wadogo wanawake. Hata hivyo inapaswa kuzingatiwa kwamba, wanawake katika uchimbaji mdogo wangechangia kwa sehemu kubwa katika maendeleo ya uchimbaji mdogo nchini Tanzania.

## Kupitia Mradi wa Jinsia, shirika la FADev limefanikisha mambo yafuatayo:

i. lilifanya utafiti wa kukusanya taarifa za awali kuhusu Wanawake katika Uchimbaji Mdogo katika mikoa ya Geita na Shinyanga

ii. lilifanya tathmini ya mahitaji miongoni mwa Wanawake katika Uchimbaji Mdogo wa Dhahabu katika mikoa ya Geita na Shinyanga

2 *Mutagwaba na wenzake 2018, Artisanal and small-scale mining in Tanzania – Evidence to inform an 'action dialogue'*. Ripoti ya utafiti, IIED, London. Ilipatikana mtandaoni kupitia: http://pubs.iied.org/16641IIED.

iii. lilianzisha uhusiano wa kazi pamoja na Makundi 15 ya Wanawake katika mikoa ya Geita na Shinyanga.

iv. lilifanya semina za uongozi kwa ajili ya Wanawake ambao ni wanachama wa wachimbaji wadogo na viongozi wa kikundi wanaowakilisha makundi 13 ya wanawake katika mikoa ya Geita na Shinyanga.

v. lilijenga uwezo wa kiujasiriamali miongoni mwa makundi 10 ya wanawake mkoani Geita

Kama sehemu ya Mradi wa Jinsia, FADev inakusudia kuendelea kutathmini mahitaji ya Makundi ya Wanawake kwenye vyama vya wachimbaji wadogo, na kukidhi baadhi ya mahitaji haya kwa kutumia fedha iliyopo.

Kwa sababu ya ukosefu wa fedha ya kutosha, Shirika linaweza kutoa yafuatayo kwa makundi yanayoongozwa na wanawake kwenye mikoa ya Geita na Shinyanga:

i. upatikanaji wa vifaa vya kazi kwa ajili ya vikundi vya wanawake wanaojihusisha moja kwa moja katika shughuli za uchimbaji mdogo. Kuhakikisha kwamba wanawake wengi wanathamini zaidi shughuli zao za uchimbaji mdogo, shirika la FADev linatoa asilimia 50 ya gharama ya manunuzi ya mitambo kama ruzuku. Kikundi hicho cha wanawake kitalipa asilimia 50 tu bila riba, na

ii. kutoa ruzuku ndogo kwa makundi ya wanawake yanayojihusisha moja kwa moja katika shughuli za uchimbaji mdogo na wale ambao wanaishi ndani ya eneo hilo na wanafanya shuguli zao ndani ya jamii za wachimbaji wadogo

FADev inaendelea kufanya kazi na wadau muhimu, ikiwa ni pamoja na Wachimbaji Wanawake na serikali kupitia wizara mbalimbali kwenye mchakato wa maboresho yanayolenga kuwajengea uwezo wanawake wanaofanya shughuli za uchimbaji mdogo. Lengo letu ni kuhakikisha tunapata masuluhisho yanayotekelezeka kuhusu changamoto za kijamii, kisheria, kiuchumi, kiufundi, kitaaluma na kisiasa zinazowakumba wanawake wachimbaji, vilevile kubainisha fursa zilizopo.




## Mwitikio wa Dharura Dhidi ya Janga la Uviko-19



Janga la ugonjwa wa Uviko-19 limesababisha changamoto zisizotarajiwa za kijamii, kiuchumi na hasa zaidi kiafya duniani kote na setka ya uchimbaji mdogo haijaachwa salama.

Katikati ya janga la virusi vya Uviko-19, FADev ilifanya tathmini ya mahitaji miongoni mwa washirika wake katika maeneo ya uchimbaji mdogo, ambayo ni: Ibondo katika Kata ya Nyaruyeye, Nyakagwe katika Kata ya Butobela katika Wilaya ya Geita, na Musasa katika Wilaya ya Chato - maeneo haya yote yapo katika Mkoa wa Geita.

Tathmini ya mahitaji ilidokeza masuala yafuatayo ambayo wanajamii wengi katika maeneo ya uchimbaji mdogo waliona kwamba ni matatizo yanayosumbua:

i. kushamiri kwa bei za kinyonyaji zinazotolewa na madalali wa madini




ii. hakuna malipo au malipo kidogo kwa wanawake wanaojihusisha katika kuchagua na kuponda mawe wakidhani kwamba wanaweza kupata dhabau iliyosalia

iii. ongezeko la gharama ya maisha

iv. kuongezeka kwa matukio ya ukatili wa kijinsia[3]

v. hitaji na ukosefu wa maji safi na salama, na

vi. hitaji la kujenga uelewa kuhusu virusi vya Uviko-19 kwenye jamii ya wachimbaji wadogo.

Kwa kutambua ufinyu wa rasilimali zake, na kutokuwa na mamlaka ya kushughulikia masuala haya bila ruhusa kutoka kwenye Wizara husika, FADev ilichukuwa hatua ya makusudi kuishirikisha kikosi kazi cha kushughulikia janga la virusi vya Uviko-19, kinachofanya kazi chini ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

Taarifa za kusahaulika kwa jamii ya wachimbaji wadogo, katika wakati huu wa Uviko-19 ilisikitisha, ukuzingatia ukweli kwamba, wachimbaji wadogo hawawezi kufungiwa ndani saa 24 bila kufanya kazi. Mfumo wao wa uchumi unategemea kufanya kazi kila siku ndipo mtu apate riziki ya siku. Hali hii inawezakupelea maambukizi makubwa ya Uviko-19 kulingana na mwingiliano mkubwa baina ya watu katika mazingira yao ya kazi.

Wachimbaji - wanawake na wanaume, wanatoka kwenda kuzitafutia familia zao riziki. Shughuli hizi zinafanywa katika maeneo ya uchimbaji mdogo yenye hatari ya juu, hivyo hitaji lao la kupata msaada wa dharura lilikuwa ni la haraka sana.

Kutokana na mashauriano na kikosi kazi kilichoundwa kushughulikia masuala

3 *Hii inarejelea kazi isiyo na malipo ambayo wanawake wengi wanaoponda mawe wanaona kama ukatili wa kijinsia*



ya Uviko-19, ilidhihirika kwamba katika mazingatio yote, hakukuwa na mkakati mzuri wa kushughulikia athari za janga la virusi vya Uviko-19 miongoni mwa jamii za uchimbaji mdogo.

Ni lazima tuseme pia, kwamba tathmini iliyofanywa na FADev kubaini changamoto kwenye jamii ya wachimbaji wadogo katika kipindi nchi imekumbwa na janga la virusi vya Uviko-19, wananchi kwenye maeneo ya uchimbaji mdogo walipata maelezo kuhusu kuchukua hatua za usafi kama ilivyoelekezwa na Wizara ya Afya. Hata hivyo, maelekezo hayo na desturi iliyokuwepo havikuendana kwa sababu ya kutokuwa na ufahamu wa kutosha miongoni mwa wananchi hao.

Tathmini hiyo ilibaini kwamba "Katika maeneo ya mradi ya FADev na pembezoni mwa barabara, kila mlango una ndoo ya maji na sabuni". Hii inazungumzia kile kilichoonekana lakini haioneshi kama wananchi walikuwa na uwezo wa kugharamikia kile kinachotakiwa kuondokana na hofu na kujikinga dhidi ya hatari ya kuambukizwa virusi vya Uviko-19.
Upatikanaji wa maji katika maeneo ya uchimbaji mdogo yalikuwa, na bado yanapatikana kwa wauziaji wa maji ambao wanatoza kati ya Shilingi 300 hadi 1,000 kwa ndoo ya lita 20. Bei zilitofautiana kulingana na eneo. Kwa mfano, katika maeneo ya Ibondo na Nyakagwe ndoo ya lita 20 za maji ilizuzwa kwa Shilingi 300 wakati wa mvua ukilinganisha na msimu wa kiangazi ambapo bei ya ujazo huo huo inauzwa kwa Shilingi 700 hadi 1000. Katika eneo la Musasa, wachimbaji wananunua ujazo huo huo wa maji kwa Shilingi 500, hata wakati wa mvua.

Katika eneo la Musasa, mchimbaji mmoja mwanamke alisema kwamba taarifa ya uwepo wa virusi vya Uviko-19 kumefanya mambo kuwa mabaya. Mwanamke mmoja alisimulia uzoefu wake akisema, "kama mwanamke, ninakabiliwa na mambo mengi. Nimeolewa na nina watoto lakini mapato yangu ndiyo ya msingi kwenye kaya yangu. Ninahitaji kuwa na maji kwenye nyumba yangu kwa ajili ya mahitaji ya nyumbani lakini sasa inakuwa ni

changamoto (ikiwa maji zaidi yanatakiwa ili kufuata taratibu za usafi). Kuna visima kadhaa hapa lakini vyote hivi ni vya taasisi nyingine. Ni lazima tununue maji. Ninawezaje kununua maji kwa ajili ya kutumia nyumbani wakati siwezi kupata fedha kama nilivyokuwa napata kabla ya korona kuwepo? Umenikuta ninafanya kazi sasa, lakini nina hofu. Unaweza kuona ninafanya kazi kwa kujitenga".

Kwa lengo la kushughulikia mahitaji ya washirika wake na yake zao, FADev uliweza kutoa vifaa vya usafi vifuatavyo: vifaa vya kujikinga - barakoa za kitambaa zinazoweza kutumika tena, na vipeperushi vyenye taarifa juu ya nini kifanywe na wananchi ili kujikinga dhidi ya maambukizi ya virusi vya Uviko-19:

| # | KIFAA | MAELEZO | IDADI | KILICHOTOLEWA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Vifaa vya Usafi | Ndoo za lita 20 zenye koki zikiwa na jina la shirika | Ndoo 70 | Zote |
| 2 | Sabuni za kuua bakteria | Sabuni za kunawia mikono za kuua bakteria | Masanduku 17[1] | Zote |
| 3 | Vifaa vya Kujikinga | Barakoa za kitambaa | Barakoa 1,500 | Zote |
| 4 | Vipeperushi vya A3 | Vipeperushi kuhusu jinsi ya kujikinga na virusi vya korona | 1,000 | Vyote |
| 5 | Vipeperushi vya A1 | Vipeperushi kuhusu jinsi ya kujikinga na virusi vya korona (ujumbe unaolenga wachimbaji wadogo). | 30 | Vyote |

### *Waliopokea vifaa*

| # | MPOKEAJI | UHUSIANO |
|---|---|---|
| 1 | Mgodi wa Kilimo Kwanza | Mshirika wa FADev |
| 2 | Mgodi wa Mohammed Mtalingi | Mshirika wa FADev |
| 3 | Mgodi wa Masasi John | Mshirika wa FADev |
| 4 | Chama cha Wanawake Wachimbaji wa Madini Tanzania (TAWOMA) | Mshirika wa FADev |

| | | |
|---|---|---|
| 5 | Chama cha Wanawake Wachimbaji Madini Geita (GEWOMA) | Mshirika wa FADev |
| 6 | Chama cha Wachimba Madini wa Mkoa wa Geita (GEREMA) | Mshirika wa FADev |
| 7 | Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Buseresere | Mdau wa Uchimbaji Mdogo |
| 8 | Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Musasa | Mdau wa Uchimbaji Mdogo |
| 9 | Ofisi ya Waziri Mkuu, Shule ya Msingi Musasa | Jumuiya ya Uchimbaji Mdogo |
| 10 | Mradi wa Uchimbaji Dhahabu wa Nsagano, Nyarugusu | Mdau wa Uchimbaji Mdogo |
| 11 | Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Ng'wasabuka | Mdau wa Uchimbaji Mdogo |
| 12 | Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Nyarugusu | Mdau wa Uchimbaji Mdogo |
| 13 | Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Nyakagwe | Mdau wa Uchimbaji Mdogo |
| 14 | Jeshi la Polisi Tanzania, Nyarugusu | Mdau wa Uchimbaji Mdogo |
| 15 | Ofisi ya Madini ya Mkoa, Mkoa wa Geita | Mshirika wa FADev |
| 16 | Kikundi cha Wanawake Wachimbaji Wadogo, Chato | Mshirika wa FADev |
| 17 | Kituo Kidogo cha Vito vya Thamani, Nyarugusu | Mdau wa Uchimbaji Mdogo |

## Kujenga Uelewa Kwenye Eneo la Kazi



Ikichukuliwa kama mchakato endelevu na ukifanywa kwa kutumia mbinu mbalimbali, FADev kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, na ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Geita kupitia Timu ya Mkoa ya Usimamizi wa Afya, ilifanya kazi ya kujenga uelewa kwa umma kwa siku tatu kuhusu Uviko-19, kwa wachimbaji wadogo na jamii zao katika mkoa wa Geita. Maeneo yaliyonufaika na elimu hii kwa umma ni eneo la uchimbaji mdogo

lililoko Msasa, Kata ya Buseresere, Wilaya ya Chato, eneo la Nyarugusu mjini na Nyakagawe, Kata ya Butobela.

Ujengaji wa uelewa ulifanywa kwa kuhusisha vyombo kadhaa vya habari katika mkoa wa Geita ikijumuisha: Shirika la Habari la Tanzania (TBC), Star TV, East African Television (EATV), Mwananchi Communications, Storm FM, na Radio Free Africa (RFA).

Mkakati uliotumiwa ulichaguliwa na watekelezaji kwa makusudi ili wawafikie wananchi wengine wa eneo la Kanda ya Ziwa na kwingineko ambao wasingeweza kuhusishwa moja kwa moja na mkakati huo wa kutoa elimu kwa umma juu ya jinsi ya kujikinga dhidi ya maambukizi ya virusi vya Uviko-19.

Kwa ujumla, ndani ya siku tatu hizo, shirika la FADev na mshirika wake muhimu, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Wazee na Watoto, ilifanikiwa kuwafikia watu zaidi ya watu 850. Idadi ya waliofikiwa inaweza ikawa kubwa zaidi nchi nzima – kwa wale waliokuwa wakisiliza redio na runinga.

| # | ENEO | MIKUTANO | WALIOFIKIWA |
|---|---|---|---|
| 1 | Musasa | 1 | 250 |
| 2 | Nyarugusu | 2[2] | 550 |
| 3 | Nyakagwe | 1 | 80 |
| | | Jumla ya waliofikiwa | **880**[3] |

Vichocheo vya ujengaji uelewa viliwezeshwa na wataalamu kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

Kwa kutambua umuhimu wa Mamlaka ya mkoa na serikali za mitaa katika mchakato wote, ziara za hisani zilifanywa kwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Geita, Mkurugenzi wa Wilaya ya Geita, na kwenye ofisi ya Mkurugenzi wa Wilaya ya Chato kabla ya timu kutoa elimu kuhusu Uviko-19 katika maeneo yaliyotajwa hapo juu.

## Stadi za Maisha: Mafunzo ya kutengeneza sabuni



Lengo la uwezeshaji wa wanawake linaweza kufanikiwa kwa njia mbalimbali, lakini uhuru wao wa kiuchumi ni nguzo muhimu ili kupunguza utegemezi wao kwa waume zao na familia zao.

Moja wapo kati ya matokeo yaliyotokana na tathmini ya mahitaji iliyofanywa na FADev ndani ya jamii ya wachimbaji wadogo katikati ya janga la virusi vya Uviko-19, ilikuwa ni hali mbaya ya wanawake kiuchumi katika mazingira ya uchimbaji mdogo wa madini.

Katika mjadala kuhusu namna ambavyo mahitaji ya kiuchumi miongoni mwa wanawake waliopo katika maeneo ya uchimbaji mdogo yanavyoweza kukabiliwa, wanawake walipendekeza kwamba "wanaweza hata kufundishwa nama ya kutengeneza sabuni kwa kuwa ni bidhaa inayohitajika" katika mazingira ya sasa.

FADev lilichukua pendekezo hili na baada ya kulichambua kwa kina, liligundua kwamba utengenezaji wa sabuni ni wazo zuri kiuchumi, rahisi kutekelezeka, na soko lilikuwepo tayari.

Aidha, wanawake waliopo katika jamii ya wachimbaji wadogo wanaweza kujipatia kipato kutokana shughuli hii bila kuacha kufanya shughuli zao nyingine zinazohusiana na uchimbaji mdogo - kwa wale ambao wanajihusisha moja kwa moja kwenye shughuli za uchimbaji mdogo.

## Unataka kujua kilichotokea?

- ✓ FADev ilitafuta na kupata mkufunzi mzuri
- ✓ wanawake 33 walipata mafunzo ya kutengeneza sabuni, na
- ✓ idadi ileile ya wanawake wanaendelea kupata fedha za ziada kutokana na utengenezaji wa sabauni kama njia ya kukabiliana na athari za kijamii na kiuchumi zilizotokea katika jamii zao kwa sababu ya janga la virusi vya Uviko-19.





## Mafanikio Makuu

Kuna mambo mengi ambayo sisi na washirika wetu tunaweza kujivunia. Lakini haya ni baadhi ya mafanikio muhimu sana:

- ✓ kuonesha umuhimu wetu katika Sekta ya Uchimbaji Madini, kwa kuweka mkazo wetu kwenye sekta ya uchimbaji mdogo
- ✓ kuanzisha uhusiano wa kiutendaji baina ya FADev na Wizara husika za Serikali, Wakala za serikali, na wadau wengine muhimu wa uchimbaji mdogo
- ✓ kuanzisha uhusiano imara wa kiutendaji pamoja na mamlaka za Serikali katika ngazi za vijiji na mkoa
- ✓ uanzishwaji wa miradi ya Migodi ya Mfano ya uchimbaji mdogo
- ✓ utekelezaji wa mfumo wa kukodisha mitambo kwa nia ya kumiliki katika Migodi mitatu ya Mfano iliyoanzishwa kama majaribio.

- ✓ kuanzisha uhusiano wa kiutendaji baina ya FADev na vyombo vya habari nchini Tanzania
- ✓ kuonesha umuhimu wa Taasisi kwenye uwanda wa Kitaifa, Kikanda na Kimataifa, hasa kwa kukubaliwa kama Mwangalizi aanyetoka Mashirika ya Kiraia katika Mkutano wa Vyama vya Mkutano wa Minamata juu ya Zebaki.
- ✓ uanzishaji wa Mradi wa Jinsia unaojikita kufanya kazi na wanawake waliopo kwenye mazingira ya sekta ya uchimbaji mdogo na jamii zao
- ✓ kuanzisha uhusiano wa kiutendaji baina ya FADev na shirika la Wanawake la Sheria na Maendeleo Barani Afrika (**WiLDAF**)
- ✓ kufanikiwa kuitikia na kutoa mahitaji ya dharura kukabili janga la virusi vya Uviko-19 katika jamii ya wachimbaji wadogo
- ✓ ushirikiano endelevu na wenye mafanikio kati ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto katika shughuli ya kujenga uelewa wa janga la virusi vya Uviko-19 kwenye jamii za wachimbaji wadogo
- ✓ kuanzisha uhusiano na wadau wengine katika sekta ya uchimbaji madini kama vile Mgodi wa Dhahabu wa Geita (GGM) wa Shirika la Uchimbaji Madini la AngloGold, kampuni ya Mantra na Shanta
- ✓ kuanzisha uhusiano na wadau wanaofanya kazi au wangependa kufanya kazi katika programu zinazoangazia sekta ya uchimbaji mdogo kama vile Programu ya Maendeleo ya Umoja wa Mataifa (UNDP)
- ✓ kuandaa rasimu ya kwanza ya Mpango Mkakati wa Taasisi ya Kuendeleza Uchimbaji Mdogo (FADev)



## Changamoto Kuu

Moja kati ya changamoto kubwa kabisa ni fedha.

Kama shirika, kuna mahitaji mengi ya raslimali fedha ambayo tunakabiliana nayo baada ya kujenga matarajio makubwa miongoni mwa jamii na wadau wa sekta ya uchimbaji mdogo. Ikizingatiwa kwamba, sekta ya uchimbaji mdogo imekuwa haijiendeshi kwa mtazamo wa kibiashara, na matokeo yake watendaji wake hawajaweza kupata fursa za mkopo wa fedha.

### Vyanzo vya Mapato vya Sasa:

Miezi kadhaa baada ya kusajiliwa mwezi Julai 2019, FADev ilipata fursa ya kupokea fedha ya kianzio kutoka SWISSAID Tanzania kwa mpangilio ufuatao:

a) Shilingi **98,135,575** kwa mwezi Septemba hadi Desemba 2019,

b) Shilingi **388,539,661** kwa mwaka 2020, na

c) Shilingi **416,413,000** kwa mwaka 2021.

Fedha hii imesaidia sana katika:

- ✓ uanzishaji wa Sekretarieti
- ✓ kununua zana muhimu za kutendea kazi ofisini
- ✓ kugharimia shughuli za uendeshaji wa Taasisi
- ✓ kulipa mishahara ya wafanyakazi, ingawa kwa kiwango cha mshahara, na mafao yote mengine, na
- ✓ kusaidia shughuli za programu ikiwa ni pamoja na
    - kufanya ziara kwenye maeneo ya uchimbaji mdogo, na gharama zinazohusika
    - kufanya mafunzo kwa wadau – wachimbaji wadogo
    - kununununua vifaa vya huduma ya kwanza na kujikinga kwa ajili ya shughuli za mradi wa Migodi ya Mfano ya uchimbaji mdogo
    - kufanya uchanganuzi wa kubaini mapengo
    - kufanya utafiti wa awali kuhusu wanawake katika sekta ya uchimbaji mdogo
    - Kuandaa Mpango wa Utunzaji wa Mazingira kwa ajili ya Migodi mitatu ya Mfano huko Ibondo na Nyakagwe katika Wilaya ya Geita, na Msasa katika Wilaya ya Chato
    - kutoa vifaa vya uchimbaji kwa mfumo wa kukodisha kwa nia kumiliki
    - kutoa ruzuku kwa makundi yanayoongozwa na wanawake katika jamii ya wachimbaji wadogo
    - kuchapisha ripoti, vipeperushi na nyenzo nyinginezo zenye maelezo ya kuelimisha kuhusu uchimbaji mdogo, na
    - kuanzisha mchakato wa kutengeneza na kusimamia tovuti ya FADev

**Mahitaji na Vyanzo vya Fedha Vilivyopo:**

Kuna uhitaji mkubwa wa fedha katika mazingira ya uendeshaji wa sekta ya uchimbaji mdogo huku kukiwa na pengo kubwa la rasilimali fedha.




## Matarajio na vipaumbele kwa miaka mitano ijayo

Katika mchakato wa kujiimarisha kama shirika, tumeweza kutengeneza mpango mkakati wa kwanza kabisa. Mpango mkakati huo umeelezea juu ya Nguzo za Kimkakati za Programu.

Mpango Mkakati una malengo halisi, mapana kwenye suala zima la shughuli za kiutekelezaji ndani ya miaka hiyo mitano (5) kadri fedha zitakavyoruhusu. Kwa moyo huo, tutafanya kazi kutekeleza shughuli zilizoainishwa chini ya nguzo tofauti za kimkakati kama ilivyoonyeshwa hapa chini:

| NGUZO LA KIMKAKATI | LENGO LA KIMKAKATI NA. 1 | LENGO LA KIMKAKATI NA. 2 | LENGO LA KIMKAKATI NA. 3 |
|---|---|---|---|
| 1. **SEKTA RASMI NA HALALI KISHERIA** | Kukuza utafiti sahihi, uchenjuaji na mbinu za kuongeza uthamini wa madini | Kukuza shughuli rasmi na za kisheria katika sekta ya Uchimbaji Mdogo wa Madini | Kuwashirikisha watunga sera kwenye juhudi zinazolenga kuboresha sheria inayosimamia sekta ya Uchimbaji Mdogo wa madini |
| 2. **SEKTA INAYOJALI MAZINGIRA NA ADILIFU** | Kukuza matumizi ya njia bora za uchimbaji na uchenjuaji kwenye mazingira | Kutoa elimu juu ya mazingira, afya na usalama katika maeneo ya uchimbaji mdogo | Kushirikisha na kuelimisha jamii za wachimbaji wadogo juu ya kukuza haki za binadamu |
| 3. **USHIRIKI WA WANAWAKE WENYE TIJA KATIKA SEKTA** | Kuhamasisha jamii ya wachimbaji wadogo juu ya athari za imani za kimila yanayozuia ushiriki wa wanawake kushiriki kikamilifu kwenye shughuli za uchimbaji mdogo wa madini | Kuwezesha uhusiano kati ya taasisi za kifedha na vikundi vya wanawake wanaofanya shughuli za uchimbaji mdogo wa madini. | Kuwajengea uwezo vikundi vinavyoongozwa na wanawake wanaofanya shughuli za uchimbaji mdogo wa madini |
| 4. **BIASHARA ENDELEVU NDANI NA NJE YA SEKTA** | Kuwezesha uhusiano kati ya taasisi za kifedha na wanawake wanafanya shughuli za uchimbaji mdogo wa madini. | Kukuza ujuzi wa ujasiriamali na upanuzi wa nyanda za biashara ndani ya jamii ya wachimbaji wadogo. | Kukuza ujuzi wa uongezaji thamani madini |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 5. **UTAFITI, MIJADALA SHIRIKISHI NA TAASISI IMARA** | Kuimarisha uwezo wa Sekretariati ya FADev | Kukuza utafiti na kuanzisha kituo ambacho kitakuwa na taarifa mbalimbali juu ya sekta ya uchimbaji mdogo. | Kuendeleza majadiliano kati ya wadau wa sekta ya uchimbaji mdogo wa madini. |



Uzinduzi wa tovuti ya FADev, Dodoma_2020


Majadiliano na wadau, Lwamgasa_2018

Sekta Rasmi na Halali Kisheria

Sekta Adilifu na inayojali Mazingira

Ushiriki wenye tija wa wanawake katika sekta ya uchimbaji mdogo

Biashara Endelevu ndani na nje ya Sekta ya uchimbaji mdogo

Mijadala Shirikishi na uimarishwaji wa Taasisi

FADev
TAASISI YA KUENDELEZA UCHIMBAJI MDOGO

## Mawasiliano

FADev, Kitalu Namba 53
Barabara ya Chole, Msasani Peninsula
S. L. P 75419, Dar es Salaam – TANZANIA.
Ofisi: +255 747 474 291
Barua Pepe: info@fadev.or.tz
Tovuti: www.fadev.or.tz

fadevtz
FADevTz
Foundation for ASM Development